

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA

20 MEI, 2024



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA – TAREHE 20 MEI, 2024**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa

Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

##### **376. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini Watumishi wa Umma watarekebishiwa Madaraja hasa Walimu waliopandishwa na kunyang'anywa Mwaka 2016 - 2018 kupisha uhakiki.

#### **WIZARA YA NISHATI:**

##### **377. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFU (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini ujenzi wa njia ya umeme ya Msongo Mkuu Tabora – Mpanda utakamilika.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **378. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Kigonsera hadi Matiri.

### **379. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Madaraja ya Bujonde na Ilondo Mwaya - Kyela utaanza.

### **380. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Kibirashi hadi Songe Kilindi kwa kiwango cha lami.

### **381. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO (SENGEREMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini mradi wa ujenzi wa Feri ya Mv. Buyagu utakamilika ikizingatiwa kuwa Mkataba wa Ujenzi umekwisha muda wake Aprili, 2024.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **382. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaanza kulipa fidia Wananchi wa Kijiji cha Ngombo waliopisha Hifadhi ya Pori Tengefu la Kilombero.

### **383. MHESHIMIWA JOSEPHINE GENZABUKE (VITI MAALUM): JOHN**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itafika katika Kata ya Kagerankanda kutatua mgogoro wa mpaka baina ya Vijiji na TFS.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **384. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji katika Kijiji cha Chemchem - Karatu.

**385. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini kibali cha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kyerwa, Nyaruzumbura, Nyakatuntu, Kamuli kitatolewa ili ujenzi uanze.

**WIZARA YA FEDHA:**

**386. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, nini msingi wa Wafanyabiashara kutoza bei tofauti au Fedha za Kigeni kwa Wateja ambao ni Raia wa Kigeni na nini athari zake.

**387. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurahisisha mfumo wa kutoa msamaha wa kodi kwa Wakandarasi wanaojenga Barabara Halmashauri ya Msalala.

## **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

### **388. MHESHIMIWA AMANDUS JULIUS CHINGUILE (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itafufua Viwanda vya Mafuta Ilulu na Kubangua Korosho - Nachingwea.

## **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

### **389. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, kuna mpango gani wa kuongeza nafasi za ajira na mafunzo Jeshini kwa Vijana wanaomaliza Darasa la Saba na Kidato cha Nne.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA**  
**20 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**

